

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA**

SHULE YA SEKONDARI SIMBO  
S.L.P 322,  
**IGUNGA-TABORA.**

10.12.2020.

Kumb.Na **HWIG/SSS/JI/VOL.1/2020/.....**

Mwanafunzi.....

Shule ya Msingi.....

S.L.P.....

**IGUNGA.**

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA I MWAKA 2021.**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga Kidato cha Kwanza katika Shule ya Sekondari Simbo, Wilaya ya Igunga , Mkoa wa Tabora. Shule ya Sekondari Simbo ipo umbali wa Kilometa 3 kutoka Simbo madukani upande wa Mashariki. Hongera sana kwa kupata nafasi hii.

Ni matumaini yangu kuwa utaipokea na kuitumia nafasi hii vizuri kwa manufaa yako, jamii yako na Taifa kwa ujumla.

Shule ya Sekondari Simbo ni ya kutwa, hivyo Mzazi/Mlezi wako atawajibika kukutafutia makazi/malazi ambayo ni salama na rafiki wa elimu.

Shule itafunguliwa tarahae 11/01/2021, unatakiwa kufika tarehe hiyo. Kwa ambao mtachelewa, mwisho wa kuripoti ni tar.18/01/2021. Aidha yakupasa kutambua kuwa, kutoripoti kwa wakati au kutoripoti kabisa, ni kosa kisheria.

**MAHITAJI MUHIMU.**

**SARE ZA SHULE**

**>WASICHANA**

- Sketi ya Kaki yenye marinda ya kupanga iwe inavuka magoti, isibane mwili na iwe na mkanda usiozidi nchi 2.
- Shati rangi nyeupe mikono mifupi lisilobana mwili lichomekewe ndani ya sketi wakati wote uwapo Shuleni au nje ya Shule. Kwa watoto wa Kiislam waweza kushonewa Blauzi yenye mikono mirefu isiyochomekewa, isiyopitisha mwanga wala kubana mwili.
- Viatu vyeusi vya kamba rangi nyeusi na vya ngozi, visivyo na urembo wala visigino virefu vyenye kutumia kiwi. Viatu nguo (Raba) haviruhusiwi hata kama ni vyeusi.
- Soksi ndefu nyeupe
- Wasichana wa madhehebu ya Kiislamu wanaruhusiwa kuvaa Hijabu wakati wa masomo ila lazima iwe nyeupe na isiwe na maua au urembo wowote.
- Tai ya shingoni (Neck tie) rangi ya Suruali/Sketi ya shule.

**>WAVULANA**

- Suruali ya Kaki yenye marinda mawili kila upande na iwe na upindo (turn up) chini. Ni mwiko kuvaa Suruali inayobana, isiyo na marinda wala upindo.
- Shati rangi nyeupe mikono mifupi lisilobana mwili. Shati lichomekewe ndani ya suruali wakati wote uwapo Shuleni au nje ya Shule.
- Mkanda uwe rangi nyeusi na uwe wa heshima
- Viatu vya ngozi rangi nyeusi vyenye kamba, na viwe na visigino vifupi.
- Soksi ndefu nyeupe.
- Tai ndefu inayofikia kitovu, iwe rangi ya suruali ya shule.

## **MICHANGO YA CHAKULA**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na michango ya chakula siku ya kuripoti. Michango hiyo ni:

- Mahindi Debe moja
- Maharage kilo tano
- Mchele kilo tano
- Sukari kilo tatu
- Fedha Tsh. 5,000/=

Michango hii ni muhimu sana kwani huwasaidia wanafunzi kupata Kifungua kinywa pamoja na Chakula cha mchana kuliko kushinda bila kula kitu chochote. Kamati ya Chakula shuleni iliyoundwa na Wazazi ndiyo inayosimamia michango hii.

## **VIFAA VYA MICHEZO**

Wanafunzi wote wa kike na kiume wanatakiwa kuwa na vifaa vifuatavyo vya michezo:

- Bukta/traki suti moja rangi nyekundu.
- Jozi moja ya viatu vya raba
- Tisheti rangi ya njano.

## **MAMBO MENGINE MUHIMU**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na fomu zifuatazo:

- Fomu ya uchunguzi wa afya yake.
- Fomu ya kukubali kusoma Shule ya Sekondari Simbo.
- Madaftari 11 mapya, Kalamu (Blue/Black), Penseli, Kifutio, Rula na Mkebe wa Hesabu (Mathematical set).

## **MAMBO YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

- 1.Wizi
- 2.Uasherati, ubakaji na ushoga.
- 3.Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevywa.
- 4.Uvutaji bangi, sigara, unga, n.k.
- 5.Makosa ya jinai.
- 6.Kupigana au kupiga (Ugomvi).
- 7.Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- 8.Kudharau bendera ya Taifa.
- 9.Kuo au kuolewa.
- 10.Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
- 11.Kutoa mimba.
- 12.Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu.
- 13.Kukataa adhabu kwa makusudi.

**KUMBUKA:** Kwa kuwa yote haya yanaepukika, jitahidi kuyaepuka kwani hatutakuwa na nafasi ya kukuvumilia kwa namna yoyote ile.

***“Kila la kheri katika maandalizi ya kujiunga na Shule ya Sekondari Simbo”***

***Karibu sana,***

.....  
**RUSHALILA, A.A**  
**MKUU WA SHULE**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
IGUNGA DISTRICT COUNCIL  
SIMBO SECONDARY SCHOOL P.O BOX 322, IGUNGA.**

**STUDENT MEDICAL EXAMINATION FORM.**

THE MEDICAL OFFICER IN CHARGE

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

**REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**FOR**.....

Please examine the above named student as to his/her physical and mental fitness for full time studying. *(This Medical Examination Form should be completed by the Government Medical Officer).*

*I have examined the above named student and findings were as follows:*

<b>NO</b>	<b>CATEGORY</b>	<b>FINDINGS</b>
1	Eye sight	
2	Hearing	
3	Limb	
4	Speech	
5	Venereal Diseases	
6	Leprosy	
7	Epilepsy	
8	Blood Test	
9	Asthma	
10	Anemia	
11	Chest	
12	Operation	
13	Stool examination	
14	T.S test	
15	Serious accident	
16	Any other infection	
17	Neuroses	
18	Pregnancy	
19	Other serious diseases	

**MEDICAL CERTIFICATION**

The diagnosis above reveals that the above named student is physically and mentally fit/unfit for full time studying.

\_\_\_\_\_  
Name of Medical Officer In Charge

\_\_\_\_\_  
Signature

\_\_\_\_\_  
Date

Official Stamp/Rubber.....

**FOMU YA KUKUBALI KUSOMA KATIKA SHULE YA SEKONDARI SIMBO.**

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi \_\_\_\_\_ ambaye ni Mzazi/Mlezi wa  
\_\_\_\_\_ Kidato cha \_\_\_\_\_ Mwaka  
\_\_\_\_\_

Nimeyasoma maelekezo/maagizo haya na kuyaelewa vema. Nimekubali mwanangu ajiunge na Shule hii. Nitashirikiana na uongozi wa Shule kuhakikisha kuwa mwanangu anahudhuria shuleni bila kukosa ikiwa ni pamoja na kutii Sheria za Shule. Endapo mwanangu atakiuka sheria/taratibu za shule, nitaunga mkono adhabu yoyote itakayotolewa dhidi yake.

**Saini ya Mzazi /Mlezi** \_\_\_\_\_

**Anuani kamili** \_\_\_\_\_

**Simu** \_\_\_\_\_

**Tarehe** \_\_\_\_\_

**AHADI YA MWANAFUNZI.**

Mimi \_\_\_\_\_ ambaye ni mwanfunzi,  
nimeyasoma maelekezo/maagizo yote na kuyaelewa. Nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii.

Ninaelewa kuwa shuleni ni mahali pa kujifunza na siyo kufanya mzaha. Ninaahidi mbele ya Wazazi/Walezi wangu kuwa nitaitumia vema nafasi hii niliyopewa kwa kushirikiana na uongozi wa shule na wanafunzi wenzangu kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote ,pia nitahudhuria shuleni bila kukosa ili niwe mfano mwema kwa wanafunzi wenzangu na jamii kwa ujumla. Kamwe sitahusika au kushiriki aina yeyote ya fujo/mgomo nikiwa shuleni na hata nje ya shule.

**Saini ya mwanafunzi** \_\_\_\_\_

**Tarehe** \_\_\_\_\_

***“Kila la kheri katika maandalizi ya kujiunga na Shule ya Sekondari Simbo”***

***Karibu sana,***

.....  
**RUSHALILA, A.A**  
**MKUU WA SHULE**